# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## BUNGE LA TANZANIA

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA TATU

## KIKAO CHA ISHIRINI NA NANE

**25 MEI, 2016**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

______________________

## MKUTANO WA TATU

## KIKAO CHA ISHIRINI NA NANE – TAREHE 25 MEI, 2016

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

## II. MASWALI:

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**229. MHESHIMIWA JOSEPH LEONARD HAULE (MIKUMI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Serikali ilifanya tathmini na kuona umuhimu wa kujenga daraja kwenye Kata ya Ruhembe kwa shilingi milioni mia sita lakini mpaka sasa ni shilingi milioni mia moja tu zimepelekwa kwenye Halmashauri ya Kilosa.

Je, ni lini kiasi cha Shilingi milioni mia tano kilichobakia kitapelekwa ili kukamilisha daraja hilo

na kuwasaidia wananchi wa Ruhembe wanaozunguka umbali mrefu ili kupata mahitaji yao.

**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

**230. MHESHIMIWA DEOGRATIAS FRANCIS NGALAWA (LUDEWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Serikali ilitoa ahadi ya kutengeneza barabara ya lami toka Itoni - Njombe - Manda na upembuzi yakinifu tayari umeshafanyika:-

Je, ni lini ujenzi huo utaanza hasa ikizingatiwa kuwa barabara hiyo imekuwa kero kubwa hasa kipindi cha masika lakini pia ni muhimu kwa sababu ya ujio wa miradi ya makaa ya mawe Nchuchuma na Chuma cha Liganga.

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

**231. MHESHIMIWA EMMANUEL PAPIAN JOHN (KITETO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:- Kwa kipindi kirefu sasa kumekuwa na migogoro mingi ya ardhi huko Kiteto baina ya Wakulima na wafugaji:-

(a) Je, ni lini Serikali itaipatia Kiteto Mahakama ya Baraza la ardhi ili kesi nyingi ziweze kusikilizwa hapo Kiteto;

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuipima ardhi yote ya Kiteto ili kila mtu afahamu mipaka ya eneo lake ili kuepusha mwingiliano wa maeneo usio wa lazima, na itafanya hivyo lini.

**232. MHESHIMIWA SALMA MOHAMED MWASSA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:- Kumekuwa na migogoro mingi ya ardhi Mijini na Vijijini inayotokana na kutopima na kutopanga matumizi bora ya ardhi:-

(a) Je, Serikali imejipangaje kupunguza au kumaliza migogoro ya ardhi;

(b) Je, ni lini Serikali itaandaa mipango kabambe (*Master Plan*) Mijini na Vijijini ili kuainisha matumizi bora ya ardhi na kuondoa migogoro ya ardhi nchini.

**233. MHESHIMIWA ALLY SEIF UNGANDO (KIBITI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:- Kuendana na kasi ya Mheshimiwa Rais kutaka kumaliza kabisa urasimu wa upatikanaji wa hati za kimila na hati miliki za ardhi mpaka sasa bado ni tatizo kwa Wilaya ya Rufiji:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka Afisa Ardhi katika Wilaya ya Rufiji;

(b) Je, Serikali haioni kwamba ina kila sababu ya kupeleka vifaa vya kisasa vya kupimia viwanja na mashamba katika Wilaya hiyo.

**WIZARA YA NISHATI NA MADINI:**

**234. MHESHIMIWA MAGDALENA HAMIS SAKAYA (KALIUA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:- Wananchi wa Kitongoji cha Twende Pamoja Kijiji cha Igwisi Wilaya ya Kaliua wamekuwa wakipata athari kubwa za kiafya kutokana na milipuko ya baruti inayofanywa na Kampuni ya CHIKO kupasua mawe na kokoto kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Kaliua mpaka Kigoma:-

(a) Je, Kwa nini Serikali isiwalipe wananchi hao stahiki zao ili waondoke sehemu hiyo na waende kuishi maeneo mengine ambayo ni salama;

(b) Je, Kijiji cha Igwisi kinanufaikaje na machimbo haya ya mawe ambayo yapo kwenye eneo hilo.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI:**

**235. MHESHIMIWA MARIAM NASSOR KISANGI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na ufundi:- Matatizo ya wanafunzi kutojua kusoma na kuandika pamoja na kutofanya vizuri katika mitihani yao mara zote lawama zinaenda kwa Walimu:-

Je, Serikali imefanya utafiti wa kina na kuona kama Mwalimu peke yake ndiye anayeweza kumfanya mwanafunzi aweze kufanikiwa katika masomo yake.

PARLIAMENT OF TANZANIA • BUNGE LA TANZANIA

## WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

## 236. MHESHIMIWA COSATO DAVID CHUMI (MAFINGA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Wavunaji na Watumishi wa Msitu wa Taifa SAO Hill wanapata huduma za kijamii na mahitaji yao katika Jimbo la Mafinga Mjini, na kwa kuwa Msimu uliopita hakuna Kijiji au mtaa hata mmoja uliopata kibali cha kuvuna msitu katika Jimbo hilo:-

(a) Je, Serikali iko tayari kutoa kibali cha kuvuna Msitu kwa kila Kijiji au Mtaa ili fedha zitakazopatikana kutokana na vibali hivyo ziweze kusaidia shughuli za kuboresha huduma za jamii kama vile kuchonga madawati na kumalizia ujenzi wa Zahanati.

(b) Je, Serikali iko tayari kutoa vibali vya kuvuna Msitu kwa vikundi rasmi vya wajasiliamali ili kuwasadia kukuza mahitaji yao na kujipatia maendeleo ya kiuchumi;

(c) Je, ni kiasi gani cha fedha kimetolewa kama sehemu ya kurejesha hisani kwa jamii kutoka kwa Kampuni za Misitu na viwanda vikubwa vya mazao ya msitu vilivyopo kwenye Jimbo la Mafinga na maeneo jirani.

## WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:

**237. MHESHIMIWA ENG. ATASHASTA JUSTUS NDITIYE (MUHAMBWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:- Katika Jimbo la Muhambwe kuna Chuo cha Wauguzi (MCH) ambacho ni muhimu sana katika sekta ya afya lakini hakina hali nzuri:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukiboresha chuo hicho na vingine vya aina hiyo ili viweze kujiendesha na kulipa wazabuni wengi ambao wanawadai.

**238. MHESHIMIWA TASKA RESTUTA MBOGO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:- Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2006 inaainisha kuwa mtu akifika umri wa miaka 18 huyo ni mtu mzima na Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 Ibara ya 13 inasema umri wa msichana kuolewa ni Miaka 15 na mvulana kuoa ni miaka 18:-

Je, ni lini Serikali itaifanyia marekebisho Sheria ya Ndoa ili watoto wa kike wasiolewe na umri mdogo kama ilivyo sasa.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

### WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:

Kwamba, Bunge sasa likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

**(*Majadiliano yanaendelea*)**

**DODOMA** — **DKT. T. D. KASHILILAH**
**25 MEI, 2016** — **KATIBU WA BUNGE**